

UHURU UK 19.

# Wakala wa Maabara kuongeza wigo ubora vyakula vya mifugo

**Na MWANDISHI WETU**

WAKALA ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), imesema katika mwaka ujao wa fedha 2022/2023, inatarajia kuongeza wigo wa kufanya vipimo vya ubora wa vyakula vya mifugo.

Imesema lengo la kufanya hivyo ni kubaini aina za sumu kuvu zinazoweza kusababisha madhara ya kiafya kwa binadamu na mifugo.

Mtendaji Mkuu wa TVLA, Dk. Stella Bitanyi, alibainisha hayo ofisini kwake jijini Dar es Salaam, alipozungumzia uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa nchini, uliofanywa na wataalamu wa Wakala huo, mwishoni mwa wiki katika Wilaya za Temeke na Ubungo.

Dk. Stella alisema wakala huo unatarajia pia kupima mabaki ya 'antibiotic' na dawa nyingine za mifugo ndani ya vyakula vya mifugo ili kuhakikisha ubora wa vyakula vya mifugo kwa kutokuwa na mabaki ya dawa zinazoweza kusababisha usugu wa dawa kwa mifugo na binadamu atakayetumia mazao yanayotokana na mifugo hiyo.

Alitoa wito kwa wazalishaji wa vyakula vya mifugo nchini na wafugaji kuhakikisha wanafikisha sampuli za vyakula katika maabara hiyo ili kupima ubora wa chakula kinachostahili kutumiwa na mifugo na malighafi zitakazotumiwa kutengeneza vyakula hivyo.

Alisisitiza kwamba matumizi ya vyakula sahihi vya mifugo ambavyo vina virutubisho vinavyostahili, vitamwezesha mfugaji kufuga kwa tija kwa kuwa mifugo itakuwa katika muda unaotakiwa kitaalamu na kufikia kiwango cha uzito unaotakiwa sokoni.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo katika Wilaya za Temeke na Ubungo, Ofisa Mtafiti wa Mifugo TVLA, Dk. Evaline Mfuru, alisema uwiano sawa wa virutubisho vinavyotakiwa katika vyakula vya mifugo kwa kiasi kikubwa hupunguza gharama za uzalishaji na kudhibiti magonjwa ya mifugo.

Baadhi ya wafugaji na wazalishaji wa vyakula vya mifugo, walisema uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo utakuwa na tija kwa kuhakikisha vinapatikana vyakula bora, ambavyo vitaleta tija kwa mfugaji na kuondoa sokoni vyakula vya mifugo ambavyo havikidhi vigezo.

TVLA ambayo iko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikifanya uchunguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo ili viwe katika viwango vinavyotakiwa kwa matumizi ya mifugo na kuleta tija kwa mfugaji.

**Uhakiki**

**LENGO**

WAKALA ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), imesema katika mwaka ujao wa fedha 2022/2023, inatarajia kuongeza wigo wa kufanya vipimo vya ubora wa vyakula vya mifugo, ili kubaini aina za sumu kuvu zinazoweza kusababisha madhara ya kiafya kwa binadamu na mifugo.

Scanned with CamScanner

# Eclat Development Foundation: Wakfu unaopambana kuelimisha wafugaji

Na Joseph Ngilisho

JITIHADA za kuinua sekta ya elimu nchini zimekuwa zikifanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi nchini.

Hata hivyo, jitihada za kuinua elimu hususani maeneo ya wafugaji zimekuwa zikikumbana na changamoto kama mila potofu, ubovu wa miundombinu na mazingira yasiyoridhisha katika baadhi ya maeneo hayo.

Maeneo ya wafugaji ni miongoni mwa yanayohitaji msisitizo mkubwa wa kuwekeza kwenye sekta ya elimu, kwa kuwa ni miongoni mwa maeneo yanayohitaji mkazo wa Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Shirika lisilo la kiserikali la maendeleo la Eclat Development Foundation ni miongoni mwa mashirika yanayofanya kazi ya kuinua elimu katika maeneo ya wafugaji, ambayo yanahitaji msukumo katika kupambana kutokomeza ujinga.

Shirika hili lililoanzishwa mwaka 2016 limekuwa mstari wa mbele kupambana kuinua elimu kwa watoto wa kike.

Mkurugenzi wake mkuu, Peter ole Toima anasema shirika tangu lianzishwe, limepambana kuwafikia na kuwagusa wanafunzi zaidi ya 17,000 ambayo ni mafanikio makubwa kwao.


"Tumefanikiwa kugusa wanafunzi 17,000 nchi nzima, haya ni mafanikio makubwa sana, kwetu katika kipindi cha miaka sita tangu kuanzishwa kwa taasisi hii, na tunajivunia sisi kama wadau wa sekta binafsi," anasema Ole Toima.

Hata hivyo, Ole Toima ambaye ni Mkuu wa Wilaya mstaafu nchini anataja baadhi ya maeneo ambayo taasisi yao imeyafikia ni pamoja na wilaya za Simanjiro, Monduli, Kiteto Kilolo, Ruangwa, Tandahimba, Karatu na Ngorongoro.

Ole Toima anaeleza kwamba asilimia kubwa ya miradi wanayoitekeleza imeleta tija na manufaa kwa nchi.

Anafafanua, kuwa katika miradi ya elimu shirika lao limefanikiwa kujenga shule 216 za msingi, 20 za sekondari, nyumba za walimu 14 na chuo cha ufundi stadi (VETA) kilichoko mkoani Manyara.

Mkurugenzi anasema shirika lao limejenga shule katika maeneo



Mkurugenzi wa Eclat Development Foundation, Peter ole Toima akionesha majengo ya shule yanayojengwa na shirika hilo.

yasiyofikika kirahisi hususani maeneo ya wafugaji ambayo mwamko wa elimu bado uko chini.

Anaeleza kuwa mbali na kutekeleza shughuli za kuinua sekta ya elimu, lakini pia wamekarabati shule ambazo miundombinu yake ni chakavu, vyoo vya shule, madarasa, nyumba za walimu, ofisi za walimu pamoja na kuweka samani ndani ya shule hizo.

Ole Toima anasema shirika lao pia mbali na kuinua sekta ya elimu, limejikita katika miradi ya afya na maji na kuanzisha programu maalumu za kuinua wanawake.

"Tumejenga kituo cha wanawake ili kuwawezesha kiuchumi, tumeanzisha vikundi zaidi ya 70 vya wanawake ili waondokane na utegemezi," anasema Ole Toima.

Anasema katika programu hiyo walianzisha idara ya wanawake yenye malengo ya kuwapa elimu ya afya, ujasiriamali, uzazi wa mpango na mitaji ya biashara.

"Tuna utaratibu wa kuwezesha vikundi hivi ambapo tunawapa mitaji kuanzia Sh milioni 2 na wanarejesha kuanzia asilimia 20 kwa awamu tatu, na hiyo pesa wanayorejesha inakwenda kwa vikundi vingine," anafafanua Ole Toima.

Anafafanua kuwa wamewapa kipaumbele wanawake kwa kuwa ni wepesi kujiunga na vikundi tofauti na wanaume, na pia ni waaminifu, na ndio wanalea familia kwa asilimia kubwa.

Kuhusu miradi ya maji, Ole Toima anafafanua, kwamba wameanzisha programu za kuchuja majitaka kwenye mabwawa wilayani Simanjiro kupitia mradi wa Paula, ilioasisiwa Ujerumani.

Ole Toima anasema wameanza kuchuja mabwawa matatu wilayani humo katika vijiji vya Sukuro, Naiti na Narakauo na maji hayo yanakuwa salama na safi kwa kunywa na kunufaisha watu zaidi ya 20,000 katika vijiji hivyo.

"Tumeanza na mabwawa matatu, tuna mitambo maalumu ya kuchuja maji na kuwa safi na salama kunywa," anaeleza Ole Toima.

Anasema shirika limejiwekea malengo ya kuondoa ujinga katika jamii ya Watanzania hususan wa kutojua kusoma na kuandika.

Anasisitiza kwamba endapo Taifa linahitaji mabadiliko ya uhakika, ni lazima liwekeze kwenye elimu, kwa kuwa ni mkombozi wa jamii.

"Tukitaka mabadiliko ya kweli ni lazima tuwekeze kwenye elimu, jamii zetu lazima zibadilike na elimu ina uwezo wa kumbadilisha mtu," anasema Ole Toima.

Mkurugenzi huyo anaeleza changamoto wanazokutana nazo katika majukumu yao, kuwa ni pamoja na suala la mahitaji kuwa makubwa kulingana na uwezo, ambapo uhitaji wa jamii umekuwa mkubwa kulingana na uwezo walionao.

Anafafanua, kwamba shirika lao linategemea kwa asilimia kubwa ufadhili kutoka kwa wahisani nje ya nchi, na hivyo kuna muda wanalazimika kusubiri fedha za wahisani ili watekeleze majukumu yao.

Hata hivyo, anasema changamoto nyingine ni ya miundombinu ambapo wanalazimika kutekeleza baadhi ya miradi nyakati za kiangazi badala ya masika, kwa kuwa maeneo mengi hayafikiki nyakati za masika kutokana na uharibifu wa miundombinu.

"Changamoto ya miundombinu ni tatizo kubwa kwetu, kuna muda tunashindwa kutekeleza miradi kutokana na ubovu wa miundombinu," anasema Ole Toima.

Hatahivyo, anafafanua kwamba zaidi ya Sh bilioni 12 zimetumika kugharimia miradi katika mikoa tisa na wilaya sita nchini katika kipindi cha miaka sita tangu kuanzishwa kwa taasisi yao.

Anaeleza kwamba ushirikiano baina ya Serikali na taasisi yao ni wa kuridhisha, kwa kuwa wamekuwa wakishirikiana na kamati za shule, wahandisi wa halmashauri na watalaamu serikalini, ambapo wamekuwa na msaada mkubwa katika majukumu yao.

Anasema lengo la miradi hiyo ni kufikishia elimu wananchi wa maeneo ya kifugaji, ambao hawafikiwi kirahisi, jambo ambalo wamefanikiwa kulitekeleza kwa kujenga takribani vyumba 260 vya madarasa.

> *"Changamoto ya miundombinu ni tatizo kubwa kwetu, kuna muda tunashindwa kutekeleza miradi kutokana na ubovu wa miundombinu."*

Scanned with CamScanner



Sayansi. Na Mpigapicha Maalumu

MWANANCHI UK 19

# 'Serikali ishughulikie mfumuko wa bei'

Ephrahim Bahemu, Mwananchi
ebahemu@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Chama cha Ukom- ozi wa Umma (Chaumma) kimeitaka erikali kutafuta njia bora ya kushu- hulikia suala la mfumuko wa bei san- ri na kuendelea kuheshimu misingi a soko huru la ushindani.

Mwenyekiti wa chama hicho, ashim Rungwe alisema juzi kuwa li ya uchumi wa nchi bado haijai- arika na mfuko wa bei unasababisha nanchi kukosa huduma muhimu a wakati na kwa bei nafuu.

Kumekuwa na ongezeko na mfumo bei katika huduma mbalimbali za mii, bidhaa na vifaa, tunaitaka ikali itafute njia bora na za kisa- kushughulikia changamoto hiyo ala ya kutumia ubabe na vitisho," ma.

wenge ambaye alikuwa akizung- a mambo tofauti yanayoendelea i alizungumzia mauaji yanay- abishwa na polisi na uhalifu gine akisema kuna haja ya kuwa me huru ya kuchunguza matukio ili kupata suluhu ya kudumu.

MIGOGORO

# Wafugaji waonywa tabia ya kuingiza mifugo hifadhini

**Mkuu wa Wilaya ya Serengeti asema Serikali haitamvulia yeyote.**

Beldina Nyakeke, Mwananchi
bnyakeke@mwananchi.co.tz

**Serengeti.** Wafugaji wametakiwa kuacha tabia ya kuingiza mifugo ndani ya maeneo hifadhi kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa na kunachangia kuwapo migongano kati ya wanyamapori na binadamu.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Dk Vincent Mashinji alieleza hayo juzi alipofungua mafunzo ya utatuzi wa migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ambayo yaliandaliwa na Shirika la Frankfurt Zoological Society (FZS).

"Sina ugomvi na wafugaji, lakini napenda kuwaambia ukweli maana watu wanafuga, lakini hawajui mifugo yao itakula nini na matokeo yake wanaingiza maeneo ya hifadhi. Serikali haiwezi kukubaliana na hali hii," alisema.

Alisema Serikali imepanga maeneo yaliyohifadhiwa, ili kuyapa ulinzi ambao unahusisha wananchi, lakini baadhi ya watu wakiwemo wafugaji wanakwenda kinyume, hivyo kuhatarisha uendelevu wa maeneo hayo.

> **NUKUU**
>
> **"Sina ugomvi na wafugaji, lakini napenda kuwaambia ukweli maana watu wanafuga lakini hawajui mifugo yao itakula nini na matokeo yake wanaingiza maeneo ya hifadhi. Serikali haiwezi kukubaliana na hali hii."**
>
> **Dk Vincent Mashinji**

Alitolea mfano wa athari za ulishaji mifugo ndani ya hifadhi kuwa ni pamoja na kutoweka wanyama aina ya faru ambao zamani walikuwa wengi katika Hifadhi ya Serengeti.

"Kutokana na kuharibiwa kwa ikolojia ya hifadhi hiyo, wanyama hao walitoweka kabla ya Serikali kufanya utaratibu wa kuanza kuwarejesha tena," alisema.

Akizungumzia mafunzo hayo yaliyohusisha vijana 21 kutoka vijiji saba, walinzi wa wanyamapori pamoja na taasisi za uhifadhi ndani ya Wilaya ya Serengeti, Meneja miradi wa FZS, Masegeri Rurai alisema tatizo la migongano ya wanyama na wananchi ni kubwa, hivyo shirika lake limeona ipo haja ya kushirikisha jamii ili itumie mbinu za kisasa na za jadi kupunguza migongano hiyo.

Alisema kuwa tatizo hilo linazidi kuenea katika maeneo ya jamii na kuwa tishio na kwamba kipindi cha nyuma wanyama walikuwa wanaogopa watu tofauti na sasa ambapo wanakuja hadi kwenye makazi na kusababisha madhara kwa mifugo, mashamba na wat.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Serengeti, Jacob Begha alisema mafunzo hayo yatasaidia kuwajengea washiriki mbinu za kuwadhibiti wanyama waharibifu kama tembo na simba ambao wamekuwa wakisababisha vifo kwa watu na mifugo pamoja na kuharibu mazao.

Scanned with CamScanner